**HOTUBA YA MHE. MIZENGO P. PINDA, (MB) WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWENYE SHEREHE YA UZINDUZI WA TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI YA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM, KATIKA UKUMBI WA NKRUMAH JUMAMOSI, TAREHE 27 JUNI 2009.**

Balozi Fulgence Kazaura, Mkuu wa Chuo Kikuu
cha Dar es Salaam;

Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba,
Mwenyekiti wa Baraza la Chuo;

Mheshimiwa Jumanne Maghembe (Mb.),
Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi;

Prof. Rwekaza Mukandala, Makamu wa Mkuu wa Chuo;

Waheshimiwa Mawaziri;

Waheshimiwa Wabunge;

Prof. John Kiango, Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili;

Waheshimiwa Viongozi wa Serikali;

Maprofesa, Wahadhiri na Wanafunzi;

Wanajumuiya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

Wageni Waalikwa;

Mabibi na Mabwana.

Kwanza kabisa napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Uongozi wa Chuo kwa kunialika na kunipa heshima hii ya kuwa Mgeni Rasmi katika **Uzinduzi wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.** Nimeelezwa kwamba Taasisi ya Taaluma za Kiswahili imetokana na Muungano wa Idara ya Kiswahili na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). Napenda niwapongeze wale wote waliohusika kuibua wazo hili na kufanikisha mchakato huu wa kuunganisha Asasi hizi mbili.

Shukrani za pekee ni kwa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kusimamia vizuri Mpango Mkakati wa Mageuzi ya Chuo hiki ambao umeleta ufanisi mkubwa sio tu katika kuongeza idadi ya Wanachuo wanaojiunga na Shahada mbalimbali hapa Chuoni bali pia katika kuunganisha Idara mbalimbali kwa lengo la kupanua wigo wa ushirikiano katika ufundishaji, utafiti na utoaji wa huduma kwa jamii. Ni katika mageuzi haya ya Chuo, ambapo Nchi yetu imepata mafanikio makubwa ya uanzishaji wa Vyuo Vikuu Vishiriki vya Changombe na Mkwawa. Vile vile, uanzishwaji wa Chuo cha Fani ya Uhandisi na Teknolojia, Chuo cha Fani ya Biashara, Chuo cha Elimu na Chuo cha Fani ya Sayansi za Jamii kilichozinduliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais Yoweri Kaguta Mseveni wa Uganda. Haya si mafanikio madogo, ni mafanikio makubwa ya kujivunia. **Nawapongezeni sana**!

## Historia ya lugha ya Kiswahili

**Ndugu Mkuu wa Chuo,**
Historia inaonyesha kwamba, Lugha ya Kiswahili ilianza takriban miaka 800-1000 iliyopita katika mazingira ya Vituo vya Biashara Ukanda wa Pwani ambako Wafanyabiashara kutoka Uarabuni, Uajemi na Uhindiwalikutana na wenyeji Waafrika. Lugha kuu ya Kimataifa ya Biashara wakati huo ikiwa ni Kiarabu. Inaonekana Lugha mpya ilijitokeza wakati wenyeji wa Pwani waliokuwa wasemaji wa Lugha za Kibantu walipopokea maneno mengi hasa ya Kiarabu katika mawasiliano yao. Sarufi na Msamiati wa Kibantu pamoja na maneno mengi ya Kiarabu yakajitokeza. Inakadiriwa kwamba, theluthi moja ya maneno ya Kiswahili yana asili ya Kiarabu. Vile vile,kando ya Kiarabu zipo pia lugha mbalimbali kama Kiajemi, Kihindi,Kireno na Kiingereza. Upo ukweli kwamba, Kiswahili kilikuwa na lahaja nyingi kutokana na lugha mbalimbali za Kibantu zilizochangia. Historia

inaonyesha kuwa tangu Karne ya 19 lugha hii ya Kiswahili ilianza kuenea Barani kwa njia ya Biashara.

**Wasemaji wa Lugha ya Kiswahili**

**Ndugu Mkuu wa Chuo,**

Utafiti unaonyesha kuwa hakuna uhakika kuhusu idadi ya Wasemaji wa Lugha ya Kiswahili. Idadi inayotajwa inatofautiana. Lakini zipo taarifa kwamba Kiswahili sasa kinazungumzwa na Watu zaidi ya milioni **259,** wengi wao wakiwa ni Watu wa Nchi za Afrika ya Mashariki, Kongo, Somalia, Madagascar, Msumbiji, Malawi, Zambia na baadhi ya sehemu za Sudan. Hata hivyo, kutokana na Sera za Nchi hizi, Tanzania pekee ndiyo iliyotilia maanani sana Kiswahili na hivyo kukikuza, kukienzi na kukifanya lugha ya Taifa. Aidha, kutokana na hali hiyo, umakini wa Kiswahili Nchini Tanzania ni mkubwa ukilinganishwa na Nchi nyingine. Hali hii imefanya Tanzania ionekane dira, mfano na kitovu cha Kiswahili.

**Kiswahili kama Lugha Rasmi Kitaifa**

**Ndugu Mkuu wa Chuo,**

Kiswahili kimekuwa lugha rasmi katika Nchi ya **Tanzania** kama Lugha ya Taifa. Nchini **Kenya**, lugha ya Kiswahili ni Lugha ya Taifa japo Kiingereza ni lugha rasmi ya Kiutawala. Nchini **Uganda**, Lugha ya Kiswahili ilitangazwa kuwa lugha ya Kitaifa tangu mwaka 2005 na katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kiswahili ni kati ya lugha nne za Kitaifa, pia ni lugha ya Jeshi katika Mashariki ya Nchi.

**Umuhimu na Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili**
**Ndugu Mkuu wa Chuo,**

Kiswahili kilikuwa lugha ya kwanza tu ya Wakazi wa Miji ya Waswahili sehemu za Pwani. Hata hivyo, baada ya kuenea, Kiswahili kimekuwa lugha ya Watu wengi Mjini hasa Tanzania ambako Watu wa makabila mbalimbali wanakutana. Inaaminika kwamba lugha ya Kiswahili ndiyo iliyojenga Umoja wa Kitaifa katika Nchi yetu ya Tanzania yenye Makabila ya lugha mbalimbali takriban **120**.

Kwa Tanzania, Kiswahili siyo Lugha tu bali ni Chombo muhimu sana ambacho kimewaunganisha Watanzania wote tangu enzi za Kupigania Uhuru. Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitumia Kiswahili kuwaunganisha Watanzania wote kudai na Kupigania Uhuru wa Nchi yetu. Lugha ya Kiswahili imeimarisha mahusiano ya Makabila na kuifanya Nchi ionekane kama ina Kabila moja badala ya Makabila takriban **120**. Kiswahili kimekuwa Nguzo Imara ya Mshikamano, Amani, Utulivu na Upendo miongoni mwa Watanzania.

Vilevile, Kiswahili kimeendeleza uwepo wa Ulinzi na Usalama Nchini kwa sababu Lugha hii imeviunganisha pamoja Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. Hakuna atakayepinga ukweli kuwa Kiswahili kimetuwezesha kuwa Taifa moja kwa kuondoa Ukabila, Udini, Ubaguzi wa Rangi, Ubaguzi wa Kijinsia na aina nyinginezo zote za Ubaguzi. Watoto wa Makabila mbalimbali wamekuwa wanasoma Shule moja kwa kuunganishwa na Lugha ya Kiswahili. Hata Shule za Dini, Seminari zimekuwa zinapokea Wanafunzi kutoka Makabila yote Tanzania bila kuweka Ubaguzi wowote kwa upande wa Lugha na Dini. Nawaomba Watanzania wote tujisikie fahari kuzungumza Kiswahili, maana ndiyo silaha ya Umoja wetu wa Utaifa.

**Ndugu Mkuu wa Chuo,**
Kuna mzaha unaosimuliwana Watani wa lugha kwamba **eti Kiswahili kilizaliwa Unguja, kilikulia Tanzania Bara, kikafa Kenya na kuzikwa Uganda!** Huu ni mzaha ambao Watani wa Lugha Wanautumia kujifurahisha. Lakini hali halisi ya Kiswahili ni kwamba kuna maendeleo makubwa katika kuendeleza Kiswahili hapa Nchini na Nje ya Nchi.

Ukweli ni kwamba, pamoja na kuwepo kwa idadi ya Watumiaji wengi wa Kiswahili Duniani, ziko pia Taasisi zinazolenga kukuza na kuimarisha Kiswahili. Baadhi ya Taaisisi hizo ni kama vile Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na Idara za Kiswahili katika Vyuo Vikuu vingine vya Kenya na Uganda. Vilevile, Tanzania kuna Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Kenya kuna Chama cha Kiswahili cha Taifa (CHAKITA). BAKITA na CHAKITA pamoja na Wawakilishi kutoka Uganda wanaandaa kuundwa kwa Baraza la Kiswahili la Afrika Mashariki (BAKAMA). Aidha Uchunguzi wa Kiswahili huendelea pia katika Idara za Vyuo Vikuu vingi Duniani.

Utafiti uliofanywa na Profesa John Kiango wa Chuo Kikuuu cha Dar es Salaam na kuchapishwa kama Makala katika Jarida la ***Nordic Journal of African Studies (2002)*** unaonyesha kwamba wakati huo mwaka 2002 Kiswahili Nchini Tanzania hutumiwa na Watu kiasi cha Asilimia **100,** Kenya Asilimia **80** na Uganda Asilimia **50**. Takwimu hizi zinaweza zikawa zimebadilika wakati huu kutokana na kasi ya kukua kwa Kiswahili katika Nchi jirani. Aidha, katika Afrika, Lugha ya Kiswahili imechukua mahali pa Lugha za Kigeni zilizoletwa na Wakoloni kama vile Kifaransa, Kiingereza, Kitalia na Kireno.

Leo, Kiswahili kimekuwa kinatumiwa katika kusambaza habari katika Vituo mbalimbali vya Redio ulimwenguni kama vile Sauti ya Amerika, Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), Radio ya Ujerumani*Deutsche Welle*, *Monte Carlo*, na Nchi nyenginezo za Uchina, Urusi na Irani. **Haya ni Maendeleo Makubwa katika Kukuza lugha hii na ambayo siyo ya mzaha.**

**Wadau wa Kiswahili**

**Ndugu Mkuu wa Chuo.**

**Tanzania ni Mdau Mkuu wa matumizi ya Kiswahili katika Afrika Mashariki na Bara zima la Afrika. Kutokana na kutambuliwa kwake, Serikali ya Tanzania imepewa dhamana na Nchi za Umoja wa Afrika ya kusimamia maendeleo na matumizi ya Kiswahili Barani Afrika katika Mikutano yake Mikuu na Mikutano mingine inayofanana na hiyo.**

**Kutokana na hali hiyo, kuanzia Julai, 2004, Kiswahili kilianza kutumiwa kwa mara ya kwanza kwenye Mkutano wa Umoja wa Afrika, Addis Ababa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika na Rais wa Msumbiji wakati huo, Mheshimiwa Joachim Chisano. Vilevile, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kukabidhi Uenyekiti wa Umoja wa Afrika tarehe 3 Februari 2009, Mheshimiwa Rais alitoa Hotuba nzuri ambayo ilikuwa imesheheni masuala mazito yanayokabili Bara la Afrika kwa lugha ya Kiswahili. Nitumie nafasi hii kuwapongeza Marais hawa kwa kuipandisha chati Kimataifa Lugha ya Kiswahili. Changamoto tuliyonayo ni kwa Viongozi wengine kuiga mfano huu na Watanzania wote kuendeleza kazi hii nzuri iliyoanzishwa na Viongozi hawa. Kukua kwa Lugha ya Kiswahili sio tu kutaitangaza Nchi yetu, lakini vilevile, kutatoa ajira kwa Walimu wa Kiswahili na Wataalam wa kutafsiri Kiswahili. Wito wangu sasa ni kuwaomba kuchangamkia fursa hii ambayo imejitokeza kwa Wakalimani na Wafasiri wa kuwezesha ufanisi wa mawasiliano katika Mikutano hii ya Umoja wa Afrika.**

**Ndugu Mkuu wa Chuo,**

**Kutumia Kiswahili katika Umoja wa Afrika, kumehamasisha sana Watu wa Mataifa mengine kupenda kujifunza Kiswahili kwa malengo ambayo siyo tu ya Mikutano bali ya kibiashara, kielimu, kiutamaduni na kiutandawazi. Kutokana na Maendeleo haya, Kiswahili, siyo tu lugha ya Watu wa Tanzania, Afrika Mashariki au Afrika peke yake, bali sasa, Kiswahili ni lugha ya Dunia. Lugha iliyovuka mipaka ya Afrika. Ziko taarifa kwamba Kiswahili sasa kinafundishwa katika Nchi za Uingereza, Ujerumani, Sweden, Finland, Uholanzi, Austria, Italia na Ufaransa zote katika Bara la Ulaya. Huko Marekani viko Vyuo zaidi ya 70 ambavyo hufundisha Kiswahili. Katika Amerika Kusini Nchini Mexico, Taasisi maarufu ya Lugha za Kigeni na Isimu inafundisha Kiswahili. Aidha, katika Bara la Asia Kiswahili kinafundishwa katika Nchi za China, Japani, Korea Kusini na New Zeland.**

**Katika Afrika, Nchi za Ghana, Nigeria, Libya, Algeria, Jamhuri ya Watu wa Kongo, Rwanda, Burundi, Uganda na Kenya zote zinafundisha Kiswahili. Kiswahili pia kinafundishwa katika Nchi za Kusini mwa Afrika kama vile Afrika Kusini, Namibia, Botswana, Zambia na Malawi. Kwa ujumla Kiswahili ni Lugha yenye Soko. Ni lugha inayoeleweka na ni lugha inayopanuka kwa kasi.**

**Juhudi za Serikali kuendeleza Kiswahili**

**Ndugu Mkuu wa Chuo,**

**Serikali inayo nia ya dhati ya kuendeleza lugha ya Kiswahili. Nakumbuka mara baada ya Uhuru mwaka 1961, Kiswahili kilitangazwa kuwa Lugha ya Taifa. Katika kuimarisha Tangazo hilo, Waziri Mkuu wa kwanza wakati ule aliagiza kuwa Kiswahili kitumike katika shughuli zote za Umma. Akitoa mfano wa utekelezaji wa Agizo hilo, tarehe 10 Desemba 1962, Rais wa Tanganyika wakati ule akiwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitoa Hotuba ya Jamhuri kwa Lugha ya Kiswahili.**

**Januari 1967 Agizo jingine lilitolewa na Makamu wa Pili wa Rais wakati huo Mheshimiwa Rashidi Mfaume Kawawa kwamba, Kiswahili kitumike katika shughuli zote za Kiserikali na**

**Kitaifa. Katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 1969/70 – 1973/74 yapo maelekezo haya "Tunaelekea katika utaratibu wa elimu ambao masomo yanafundishwa kwa lugha ya Kiswahili...... Hasa jinsi Serikali inavyoendelea kutumia Kiswahili katika kazi zake.......... haifai kutoa mafunzo katika Sekondari na Shule za Juu zaidi kwa lugha ya Kiingereza........**

**Aidha, Tarehe 30 Desemba 2005, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Tanzania akifungua rasmi Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema na nanukuu:**

***"Lugha ya Kiswahili imeanza kupata umaarufu Afrika na Duniani. Umoja wa Afrika umekubali Kiswahili kuwa moja ya lugha zake kuu. Aidha, Nchi za Kanda ya Maziwa Makuu zimekubali kutumia na kuendeleza Kiswahili. Serikali ya Awamu ya Nne itahakikisha kuwa juhudi hizi zinaendelezwa na kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inakua Nje ya Mipaka ya Afrika"*** **Mwisho wa Kunukuu.**

**Kwa maneno haya ya Mheshimiwa Rais, na Matamko mbalimbali ya Serikali yaliyotolewa tangu enzi za Uhuru, ni dhahiri kwamba, Kiswahili kina nafasi nzuri ya kupanuka na kushiriki katika ujenzi wa Jamii ya Watanzania na Jamii mpya ya Afrika ya Mashariki na hata Duniani kote.**

**Ndugu Mkuu wa Chuo,**
**Hapa Tanzania, sisi ni kitovu na lugha ya Kiswahili. Tumefanya mengi katika kukuza na kukiendeleza Kiswahili. Kwa mfano, Wanafunzi wanaosoma Kiswahili kama somo lao kuu katika Vyuo Vikuu (yaani wanasoma Isimu na Fasihi) wamekuwa wakiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Wanafunzi wa Mwaka wa Kwanza waliosajiliwa katika Vyuo Vikuu kwa mwaka 2005 walikuwa 259, mwaka 2006 Wanafunzi480, mwaka 2007 Wanafunzi 500, mwaka 2008 Wanafunzi 650 na mwaka 2009 Wanafunzi 500.Wanafunzi wa Shahada ya Uzamili wameongezeka kama ifuatavyo: mwaka 2005 Wanafunzi 19, mwaka 2006 Wanafunzi 16, mwaka 2007 Wanafunzi 20, mwaka 2008 Wanafunzi25 na mwaka 2009 Wanafunzi 30. Kwa upande wa Shahada ya Uzamivu, kumekuwa na Wastani wa Wanafunzi Watatu kila mwaka.**

**Ndugu Mkuu wa Chuo,**
**Ninayo taarifa kwamba hivi sasa Kiswahili kinafundishwa katika Vyuo Vikuu Vishiriki vya Changombe na Mkwawa. Kiswahili kinafundishwa pia kwenye Vyuo Binafsi kama vile Mtakatifu Augustino, Chuo Kikuu cha Tumaini- Makumira na Chuo Kikuu cha Dodoma. Katika Vyuo hivi vyote, Walimu wanaofanya kazi huko walitoka katika Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Vilevile, Walimu wengi wanaofundisha Kiswahili katika Vyuo Vikuu mbalimbali Duniani, ama walisoma Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam au walifundishwa na Walimu kutoka Taasisi hizi za Kiswahili zilizojiunga kuipata Taasisi ambayo leo hii ninaizindua. Ni dhahiri kwamba Serikali imejenga mazingira mazuri kwa Taasisi hizi ambazo zimetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya Kiswahili Duniani. Nitumie nafasi hii kuwapongeza wote walioshiriki katika kuchangia mafanikio haya.**

**Matarajio yetu ni kwamba, Taasisi hii inayozinduliwa leo itaendelea kushirikiana vizuri na Serikali kuwa chimbuko la kutoa maarifa na utaalamu wa juu wa Kiswahili kwa Nchi mbalimbali Duniani. Vilevile, kuwapatia majarida, vitabu mbalimbali na vifaa vya kisasa vya kufundishia Kiswahili kwa ngazi zote za Elimu. Tunatarajia Taasisi hii mpya ya Taaluma za Kiswahili itaongoza katika maendeleo ya Taaluma ya Kiswahili na kuwa Taasisi ya mfano, Kitaifa na Kimataifa katika ufundishaji, utafiti na utoaji wa huduma kwa jumla.**

**Changamoto**
**Ndugu Mkuu wa Chuo,**
**Pamoja na mafanikio haya yanayoonekana, sisi kama Nchi tunazo Changamoto nyingi zinazokabili lugha ya Kiswahili:**

**Kwanza: Serikali inakabiliwa na changamoto kubwa kuhusiana na dhamana iliyopewa na Umoja wa Afrika ya kusimamia maendeleo na matumizi ya Kiswahili Barani Afrika. Kuna baadhi ya Nchi za Duniani zinazoiomba Serikali ya Tanzania iwapelekee Wataalamu wa Kiswahili wa kwenda kufundisha katika Shule zao za Kati, Sekondari na Vyuo Vikuu. Nchi zinazohitaji Walimu ni nyingi, lakini nitataja Nchi chache kama vile, Namibia, Nigeria,**

Libya, Ghana, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda, Burundi, Msumbiji, Japan, Korea ya Kusini na Marekani.

Mpaka sasa bado Tanzania haijaweza kupeleka Walimu wa Kiswahili wa kutosha katika Nchi hizo kutokana na ukweli kwamba hata sisi hapa Tanzania bado hatuna Walimu wa Kiswahili wa kutosha wa kufundisha katika Shule zetu za Sekondari, Vyuo vya Ualimu na Vyuo Vikuu. Hii ni changamoto siyo tu kwa Serikali bali pia kwa Vyuo Vikuu vinavyoandaa Wataalamu wa Kiswahili.

Pili: Kiswahili ni lugha inayokua katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na inafundishwa kama somo katika Vyuo Vikuu vya Nchi hizi. Hii ina maana kwamba Wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanatambua umuhimu wa lugha hii ya Kiswahili kwa watu wake.

Tunayo Changamoto ya kuzihamasisha Serikali za Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya za Kimataifa, Makampuni mbalimbali Nchini zikiwemo Jumuiya ya Wafanyabiashara Wakuu Nchini, kuvisaidia Vyuo Vikuu hivi viweze kudahili Wanafunzi wengi iwezekanavyo wa kusoma Kiswahili katika Shahada za Kwanza, Shahada za Uzamili na Uzamivu. Ni dhahiri kwamba Serikali peke yake haiwezi kutoa Wataalamu wa Kiswahili wa kutosha kwa matumizi ya Ndani na Nje ya Nchi. Hivyo, hatuna budi kushirikiana katika kukabiliana na Changamoto hii.

Tatu: Bado kuna maeneo mengi yanayohusu Taaluma ya Kiswahili ambayo hayajafanyiwa utafiti wa lugha. Utafiti ndio uhai wa Taaluma na chimbuko la maarifa mapya. Ni kazi ya Wataalamu wa Kiswahili kufanya tafiti za kina ambazo zitakifanya Kiswahili kitumiwe siyo tu katika Mikutano ya Umoja wa Afrika bali pia katika Mikutano ya Umoja wa Mataifa. Hili linawezekana kwa kuweka juhudi kama Wataalamu wa Kiswahili mkishirikiana kwa karibu na Wakuu wa Mataifa mbalimbali.

Nne: Vyuo Vikuu vilivyoanzishwa vinaweza kufundisha Wanachuo wa Shahada ya Kwanza, lakini hawana Wahadhiri wa kutosha wa kufundisha mafunzo ya Uzamili na Uzamivu. Tunalo jukumu la Kuanzisha Programu za Shahada za Uzamili na Uzamivu zitakazokidhi mahitaji hayo kwa lengo la kukabiliana na changamoto zilizo mbele yetu.

Tano: Nimeambiwa hapa Nchini hakuna Chuo Kikuu kinachotoa mafunzo ya Ukalimani. Watu wanaohitaji stadi hii ya ukalimani wanalazimika kwenda kusomea katika Vyuo Vikuu vya Nje ya Afrika Mashariki. Hivi hili nalo tunalikubali wakati Lugha ni yetu! Hivi hatuwezi kwa kuanzia, kutumia Vyuo Vikuu na Vyuo vingine tulivyonavyo kufanya kazi hii ya kufundisha Wakalimani? Kwani lazima tuwe na Chuo kinachojitegemea kufanya kazi hiyo? Vilevile, hata kukiwepo na Wakalimani, bado hatuna Kumbi za kisasa zenye vifaa vya kusikilizia Tafsiri za Lugha mbalimbali kama ilivyo katika Ukumbi wa Kimataifa wa Arusha (AICC). Kumbi nyingi tunazofanyia Mikutano hazina Vifaa hivyo. Fani ya Ukalimani ni muhimu hasa wakati huu ambapo Kiswahili kinatumika sana katika mawasiliano ya Viongozi wa Serikali, katika Mikutano na Warsha mbalimbali zinazofanyika Ndani na Nje ya Nchi. Changamoto tulio nayo kama Nchi na hasa Wawekezaji wa Kumbi za Mikutano ni kuhakikisha Kumbi zinazojengwa na zilizopo zinakuwa na Vifaa vya kutoa huduma ya Ukalimani, ili tuweze kutumia fursa hiyo katika kukuza Lugha yetu ya Kiswahili.

Mimi napata shida sana kuona Warsha yenye Wageni wasiozidi Kumi na Waswahili 200 inaendeshwa kwa lugha ya Kiingereza, tena bila kujali kama Waswahili hao wanaelewa Kiingereza au la. Wanachojali ni kuwafurahisha Wageni Watano. Kwa maoni yangu hii ni kasumba isiyo na maelezo. Changamoto iliyo mbele yetu ni kuondoa kasumba hii kwa kupenda kutumia lugha yetu ya Kiswahili wakati wote. Aidha, upo umuhimu wa kuanzisha mafunzo haya ya Ukalimani katika Taasisi hii mpya. Lakini ni lazima iendane na nia ya dhati ya kujenga Kumbi zenye Vifaa vya kutolea huduma hii.

Kiswahili katika Teknolojia ya Kisasa
Ndugu Mkuu wa Chuo,
Ili kuwezesha lugha ya Kiswahili kutumika kikamilifu katika maeneo yake, kunatakiwa juhudi za pamoja baina ya Serikali na Wataalamu ambao ni wakuzaji lugha hii. Kwa upande wa Wataalamu wa lugha, tumeshuhudia Kiswahili kikikuzwa na kutandazwa katika Mifumo ya

**Kompyuta - Wataalam Wanaiita *Linux* na *Microsoft.* Nimeambiwa pia kwamba kama njia mojawapo ya kuboresha matumizi ya Kiswahili sanifu, tayari Wataalamu wa lugha kwa kushirikiana na Wataalamu wa Kompyuta wameweza kutengeneza Programu Maalum ya Kisahihishi cha Lugha ya Kiswahili katika Kompyuta ambayo inatumiwa kusahihisha maneno ya Kiswahili. Haya ni maendeleo makubwa yaliyofikiwa ya kukiingiza Kiswahili katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano Duniani.**

**Hitimisho**
**Ndugu Mkuu wa Chuo,**
**Nihitimishe hotuba yangu kwa kukiri kwamba, tunaweza kuongea mengi ya nadharia kuhusu lugha yetu nzuri ya Kiswahili. Tunatakiwa sasa tuanze kutekeleza hayo mengi kwavitendo. Napenda kuhimiza Taasisi hii mpya iweke juhudi zote katika kukuza Lugha ya Kiswahili ili kiweze kutumika katika nyanja zote za mawasiliano ikiwemo Sayansi na Teknolojia.Tumejifunza mengi kuhusu Kiswahili. Kiswahili kinaleta umoja, Kiswahili ni lugha nyepesi kujifunza, Kiswahili kina ladha kuongea.**

**Mwandishi na Mshairi wa Riwaya Bwana Shaban Rorbert (1909 – 1962) aliandika kuhusu lugha ya Kiswahili na kukifananisha na ladha ya Titi la Mama. Aliandika na nanukuu:**
***Titi la Mama litamu, hata likiwa la Mbwa, Kiswahili naazimu, sifayo iliyofumbwa,***
***Kwa wasiokufahamu, niimbe ilivyo kubwa, Toka kama mlizamu, funika palipozibwa, Titi la Mama litamu, jingine halishi hamu.***

***Lugha yangu ya utoto, hata sasa nimekua, Tangu ulimi mzito, sasa kusema najua, Ni sawa na manukato, moyoni mwangu na pua, Pori bahari na mto, napita nikitumia,***
***Titi la Mama litamu, jingine halishi hamu.***

**Anachosema Bwana Shaaban Robert ni kuonyesha thamani ya Kiswahili jinsi kilivyo na utamu wa aina yake katika matumizi. Historia ya Shaaban Robert, tunaambiwa alithubutu kulikataa kabila lake la Kiyao na kujiita Mswahili kuonyesha jinsi alivyokipenda Kiswahili. Alikienzi, alikisifu na kukithamini. Upo ukweli kwamba, Kiswahili kinapendwa na wengi. Ni Lugha yenye manufaa. Tujivunie Kiswahili, tukipende, tukitumie, tukienzi na tukithamini.**

**Ndugu Mkuu wa Chuo,**
**Napenda nimalizie kwa kuwapongeza tena Wanajumuiya ya Chuo Kikuu kwa Mpango Mkakati wa Chuo, wa kuunganisha Idara ya Kiswahili na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili na kuunda Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.**

**Napenda kurudia kuushukuru Uongozi wa Chuo kwa kunialika kuja kuzindua Taasisi hii ambayo imeweka historia ya pekee katika Nchi yetu ya kukuza Kiswahili. Tudumishe Kiswahili, Tudumishe Utamaduni wetu. Aidha, tutumie Taasisi hii ya Taaluma za Kiswahili kwa manufaa ya Wananchi wetu na Taifa letu.**

**Ndugu Mkuu wa Chuo, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,**
**Kwa maneno hayo machache napenda kutamka kwamba niko tayari sasa Kuzindua Rasmi Taasisi ya Taaluma za Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.**

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**